D10

ISSN 0856 - 034X

*Supplement No. 29* *24th July,2009*

# *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.30 Vol. 90 dated 24th July, 2009*

Printed by the Government Printer, Dar es salaam by Order of Government

Tangazo la Serikali Na. 245 la tarehe 24/07/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

---

## SHERIA NDOGO

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7)*

---

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI, 2009

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi za mwaka 2009 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

3. Katika sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo, maneno yafuatayo yatakuwa na maana ya:

"Afisa Muidhinishwa" maana yake ni mtumishi ye yote wa Halmashauri ambaye atateuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Gulio" maana yake ni eneo au sehemu yo yote ya wazi, au iliyojengwa, ambayo imetengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao na bidhaa zingine za viwandani kwa siku maalum;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, au Afisa ye yote wa Halmashauri atakayeteuliwa kushika na kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yo yote inayojishughulisha na ununuzi wa mazao katika eneo la Halmashauri kwa nia ya kufanya biashara;

"Muuzaji" ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yo yote inayojishughulisha na uuzaji wa mazao katika eneo la Halmashauri.

4.–(1) Kila mnunuzi atatakiwa kununua mazao kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(2) Kila mnunuzi atasaini mkataba na Halmashauri ambao utamruhusu kununua zao husika kutoka kwa wazalishaji waliomo katika eneo la Halmashauri.

5. Baada ya kusaini mkataba kwa mujibu wa kifungu cha 3(2) cha Sheria Ndogo hii mnunuzi atapewa kibali kama kinavyoonyeshwa kwenye nyongeza Na. 1 ya Sheria Ndogo hizi.

6. Ni marufuku kwa mnunuzi ye yote kununua mazao katika eneo la Halmashauri bila kuwa na leseni halali ya biashara.

7. –(1) Mnunuzi anayedaiwa ushuru wa msimu uliopita atatakiwa kulipa deni lake lote kabla hajapewa kibali kwa ajili ya ununuzi wa mazao kwa msimu unaofuata;

(2) Mnunuzi ambaye ana wasaidizi atawajibika kuwatambulisha rasmi wasaidizi wake kwa Halmashauri kabla ya kupewa kibali, na nakala halisi ya majina na picha za wasaidizi hao, ikiwa ni pamoja na saini zao itatunzwa na Halmashauri kwa kipindi chote cha msimu husika;

(3) Litakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa msaidizi wa mnunuzi kununua mazao bila maagizo au usimamizi wa mnunuzi;

(4) Ununuzi utafanyika kwa mzani au kipimo cho chote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri au mamlaka nyingine iliyowekwa kisheria.

8.–(1) Kila mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru kwa kiwango cha asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia mazao shambani,



(3) Ni marufuku kwa msafirishaji ye yote kupokea au kusafirisha mazao ambayo hayakulipiwa ushuru kwa kiwango kilichotajwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria Ndogo hii.

9. Mzalishaji ye yote ambaye kwa makusudi atamsaidia mnunuzi kukwepa ushuru atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii.

10.–(1) Mazao yote yatauzwa katika magulio ya Halmashauri yaliyowekwa kisheria na ambayo yanaonyeshwa katika nyongeza Na. 2 ya Sheria Ndogo hii, isipokuwa mazao ya maliasili na misitu ambayo yanaweza kuuzwa mahali pengine kwa ridhaa ya Mkurugenzi;

(2) Mzalishaji ye yote anayekusudia kuuzia mazao yake shambani au sehemu nyingine ambayo si gulioni atawajibika kuomba kibali kwa maandishi kutoka kwa Mkurugenzi ndani ya miezi miwili kabla ya msimu wa mavuno ya zao husika.

11.–(1) Kutakuwa na stakabadhi zilizohakikiwa na Halmashauri na kila mnunuzi atatumia stakabadhi hizo wakati wa ununuzi wa mazao;

(2) Vitabu vya stakabadhi vilivyotajwa chini ya kifungu hiki vitatolewa na kuanza kutumika kwa malipo kwa mnunuzi siku ya kukabidhiwa kibali cha kununua mazao.

12.–(1) Kila msafirishaji atalipa ada ya usafirishaji ya shilingi elfu moja (1,000) kwa kila tani moja ya mazao inayopakiwa magulioni, mashambani au sehemu yo yote nyingine ambapo uuzaji umefanyika;

(2) Endapo Mzalishaji ameamua kusafirisha mazao ili kuyauzia nje ya eneo la Halmashauri atawajibika kulipia asilimia tano (5%) ya bei ya zao hilo katika soko anakoenda kuuzia, na pia atalipa ada ya usafirishaji kwa kiwango kinachotajwa chini ya kifungu hiki.

13.–(1) Utakuwa ni wajibu wa mlipaji kuhakikisha anapewa stakabadhi halali ya malipo yo yote anayofanya;

(2) Itakuwa ni haki ya mlipaji kuonyeshwa kitambulisho na Afisa wa Halmashauri kabla ya kulipa ada au ushuru wo wote.

14. Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumuagiza mnunuzi au mzalishaji ye yote aandae na kukabidhi kwake taarifa ya kiasi cha mazao alichozalisha au kununua katika kipindi kinachotajwa katika agizo hilo.

(a) ni marufuku kuuza, kununua na pia kusafirisha mazao kabla ya saa kumi na mbili (12:00) alfajiri;

(b) ni marufuku kuuza, kununua na pia kusafirisha mazao baada ya saa kumi na mbili (12:00) jioni.

16. Msafirishaji ye yote atakayepatikana na hatia ya kusafirisha mazao yasiyolipiwa ushuru kwa mujibu wa vifungu vya 7(1) (3) na 11(1) vya Sheria Ndogo hii atalazimika kulipa fedha zote chini ya vifungu vilivyotajwa, pamoja na faini ya asilimia shirini na tano (25%) ya fedha hizo au kifungo cha miezi kumi na miwili (12) jela.

17. Isipokuwa mahali ambapo kifungu kimetaja wazi, adhabu ya mtu atakayevunja Sheria Ndogo hii itakuwa faini isiyozidi laki tatu (300,000/=) au kifungo cha miezi isiyozidi minane jela.

NYONGEZA

KIBALI CHA KUNUNULIA MAZAO

SEHEMU YA KWANZA

Jina la Mfanyabiashara .................................................... Umri ..................

Jinsia (Me/Ke) .......................................................................................

Anuani: Box ...................... Tel;No ...................... Fax .................. E-mail ..................

Aina ya zao analonunua:

Kiasi kinachotarajiwa kununuliwa: Gm .................. Kg .................. Tani ..................

Mahali mazao yatakaponunuliwa ..................................................................

Namba ya Leseni .......................................................................................

Namba ya Kibali ...................................................................................

Mnunuzi amewahi/Hajawahi kukwepa kulipa ushuru

Mimi ..................................................................... Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa juu zikinihusu mimi mwenyewe au kampuni iliyoniajiri kwa cheo cha ................................ ni za kweli tupu, na kwamba niko radhi zitumike dhidi yangu kama ushahidi mahakamani au katika chombo cho choe cha sheria.

Sahihi ........................................ Tarehe ..................................



MAONI/MAAMUZI YA MKURUGENZI

Nimeridhika na maelezo ya mwombaji, kwa hiyo nimempatia kibali hiki ambacho kitakuwa halali kuanzia leo tarehe ................................ hadi tarehe ........................... ukiwa ni msimu mmoja wa mavuno wa zao la ................................

Ninatumaini kwamba mwombaji atatekeleza majukumu yote mengine chini ya Sheria Ndogo hii.

Jina:................................................ Saini ................................................

Cheo:................................................ Tarehe: ................................................

Lakiri ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2007 na nembo hiyo iligongwa mbele ya:-

BIBI KUDRA J. MWINYIMVUA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

L.S.

MHE: SALIM M. KIBONGE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

NAKUBALI,

Dodoma,
18 Mei, 2009

MHE: MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*